UDHIBITI WA VISUMBUFU VYA MINAZI

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA-TARI

Utangulizi

Tija ya zao la minazi huweza kupungua asilimia 50 – 100% kutokana na visumbufu vikuu vya minazi. Hivyo udhibiti wa visumbufu vya minazi ni muhimu ili kuleta tija ya zao la minazi

Aina za Visumbufu

1. Wadudu – (a). Chonga wa minazi

Ni wadudu waharibifu wa zao la minazi ambao hushambulia minazi yenye umri mdogo chini ya miaka mitano. Majani yaliyoshambuliwa yana dalili za kukatwa na kuwa na alama ya 'V'. (**Picha 1**)



Picha 1: Mdudu chonga wa minazi (A), na athari zake (B)

Udhibiti wa mdudu chonga

Kuharibu mazalia ya chonga kwa kuondoa magogo ya minazi na kuyatumia kama kuchoma mkaa, mbao na vyombo vya samani. n.k.

- kuwaondoa chonga kwenye mnazi kwa kutumia ndoano na kuwaua (**Picha 2**).

Picha 2: kuondoa chonga kwa kutumia ndoano

(b). Mbu wa minazi

Mbu wa minazi ni kisumbufu hatari husababisha vidaka kudondoka. Madhara yanaweza kuwa makubwa inaweza kuwa asilimia 100% hivyo ukavuna 0.

Hufyonza majimaji kwenye vidaka na kusababisha vidaka kuharibika na kudondoka vikiwa na umri wa mwezi 1 mpaka miezi 5. (**Picha 3**)



Picha 3: Mbu wa minazi (A), nazi iliyoharibiwa na mbu wa minazi (B)

Udhibiti wa mbu wa minazi

- Ili kumdhibiti mbu wa minazi tumia mdudu majimoto kwa kufunga kamba kutoka kwenye minazi kwenda kwenye michungwa au miembe na kamba hiyo unaichovya kwenye sukari ili majimoto waweze kupanda juu ya minazi kuwala mbu hao na mayai yao.
- Kutumia viatilifu vya kuua wadudu kwa minazi mifupi; tumia cyhalothrin 5% EC mara moja kwa mwezi
- Faida ya mazao mchanganyiko wa miembe, minazi hutupatia wadudu rafiki ambao ni majimoto ambao hupunguza wadudu wasumbufu kwenye minazi.

(c). Utitiri wa minazi

Utitiri wa minazi ni wadudu ambao hupunguza ubora wa nazi kwa kufyonza maji kwenye vidaka na husababisha nazi kusinyaa **(Picha 4)** na hatimaye nazi kuwa na ganda gumu kutopanuka na kuwa nazi ndogo.

Picha 4: Athari za utitiri wa nazi

2. Kisumbufu Magonjwa - Ugonjwa wa mnyauko

Ugonjwa wa mnyauko ni tatizo linalosababishwa na vimelea aina ya phytoplasma ni tatizo sugu hapa nchini kwani husababisha hasara na hupunguza tija ya zao la mnazi kwa asilimia 100.

Dalili za ugonjwa wa mnyauko

- Kuanguka kwa vidaka (nazi changa).(pic 5a)
- Makole ambayo hayajafungua huwa meusi.(pic5b)
- Majani machanga kubadilika rangi kuwa ya shaba.
- Kuoza kwa jani la kileleni (spearleaf) na kuoza kwa mizizi na hatimaye kufa kwa mnazi. **(Picha 5).**

Picha 5: Kuanguka kwa vidaka (a) kole kuwa jeusi (b)

Udhibiti wa mnyauko wa minazi

- Unashauriwa kupanda mbegu zilizodhibitika kuwa na ukinzani dhidi ya ugonjwa wa mnyauko wa minazi kutoka chanzo kinachoaminika (TARI).
- Fuata kanuni bora za kilimo cha minazi kwa kuweka shamba safi wakati wote
- Kagua shamba lako kuangalia dalili za ugonjwa wa mnyauko na ile minazi inayoonyesha dalili ikatwe .
- Kupata mavuno mengi inawezekana **(picha 6)** kama mkulima akizingatia ushauri wa kitaalam katika udhibiti wa visumbufu vya minazi.

Picha 6: Mnazi uliotunzwa huzaa vizuri

Mawasiliano: Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Mikocheni, simu +255 22 2700552, Barabara ya Coca Cola, kitalu Na.22, Dar es Salaam, Email: cmmikocheni@tari.go.tz / www.tari.go.tz